

KCSE MOCKS

KISWAHILI PAPER 2

Consists 3 KCSE Mock set Exams.
(Class of KCSE March 2021)

For Marking Schemes Contact Mr Machuki
0795491185

Kenya Educators Contacts:

+254795491185

kenyaeducators@gmail.com

**For more e-learning resources contact Kenya
Educators via the contacts above.**

FOR MARKING SCHEMES CALL/TEXT/WHATSAPP 0795491185

PRE-MOCK 1

JINA..... NAMBARI YAKO.....

DARASA SAHIHI YAKO.....

102/2

KISWAHILI

KARATASI LA PILI

(LUGHA)

MUDA: SAA 2 ½

KCSE PRE-MOCK 1

MAAGIZO:

1. Hii karatasi ina kurasa kumi na moja zilizopigwa chapa.
2. Mtahiniwa anapaswa kukagua hii karatasi ili kuthibitisha kuwa kila ukurasa umepigwa chapa na kuwa hakuna swali linalikosekana
3. Jibu maswali yote.
4. Andika majibu katika nafasi uliyotengewa baada ya kila swali.
5. Majibu yote yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili sanifu.

KWA MATUMIZI YA MTAHINI PEKEE

SWALI	UPEO	ALAMA
1	15	
2	15	
3	40	
4	10	
JUMLA	80	

1. UFAHAMU (ALAMA 15)

Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswali:

Miaka mingi ya kutawaliwa na wakoloni iliwafanya wananchi wengi kupuuza umaarufu na uadilifu wa lugha ya Kiswahili kama lugha ya taifa kwa manufaa ya kuarifiana habari mbalimbali kwa ufasaha na kuelewana vyema.

Wakoloni pia waliwashawishi wananchi waone, kwamba lugha ya Kiswahili ni kwa ajili ya watu wale wasiokuwa na elimu na kwa wale ambao hawajastaarabika. Kwa wale wenye ‘elimu ya wastaarabu,’ wakoloni waliwashawishi kuamini kwamba lugha ya kigeni, yaani Kiingereza, ndiyo hasa lugha inayofaa kwa kujieleza na kufahamishana habari.

Kutokana na vikwazo hivi si ajabu kuona hadi hivi sasa, mwananchi halisi akijitwaza kwamba hawezi kujieleza kwa ufasaha au kumpasha mwenzie habari kwa ukamilifu mpaka atumie lugha ya Kiingereza. Hata katika maofisi mengi ya serikali, hadi hii leo, japo imeshapitishwa kwamba Kiswahili ndiyo lugha ya taifa bado utawaona wananchi wengine wanapendelea kuzungumza Kiingereza wao kwa wao, ili wajulikane kwamba wana kisomo na wamestaarabika.

Vikwazo vya namna hii vimewalemea wananchi vile vile kwa upande wa magazeti. Utaona mwananchi ambaye anafahamu Kiingereza kidogo sana, akijinunulia gazeti kubwa la Kiingereza na kuanza kuzurura nalo kutwa nzima bila kuambulia mengi ndani yake. Pia utawasikia wananchi wengi wakijidai kwamba hawataki kusoma magazeti ya Kiswahili kwa sababu inakuwa vigumu kwao kuelewa mambo yaliyomo kama vile ambavyo wangelielewa katika gazeti la Kiingereza.

Mabeberu wameshagundua kwamba tunao upotovu wa aina hiyo, ndipo utaona mara nyingi wanawaletea wananchi magazeti mengi ya Kiingereza, mengine yakiwa na nia ya kuwapotosha wakijua kwamba watayasoma tu, mradi yameandikwa kwa lugha ya Kiingereza.

Mara nyingi taifa fulani la kibeberu likitaka tuchukiane na taifa jingine ambalo ni adui yake kisiasa au kiuchumi, taifa hilo la kibeberu linaandika habari za uchochezi kwenye magazeti yao kwa lugha ya Kiingereza, mambo kuhusu taifa lile adui yake (ambalo si adui yetu).

Magazeti hayo huandikwa kwa lugha nadhifu ya Kiingereza na kuletewa wananchi hapa nchini. Maskini wananchi wengine waliotopea kwa kudhani Kiingereza ndicho lugha nzuri ya Kigazeti, wanayanunua mara moja na kuanza kuyasoma magazeti hayo, na pia kuwapa watoto wao wayasome. Matokeo yake ni kwamba, bila kujitambua, wanajikuta wanayafanya yale mabeberu waliyotarajia wayafanye, yaani wanaanza kuchukiana bure na taifa lile ambalo ni adui wa mabeberu hao, lakini si adui zetu. Madhumuni ya kuandika habari kwenye magazeti, ni kutaka kuwafahamisha wasomaji mambo yaliyotokea au yatakayotokea siku hata siku, kwa lugha inayofahamika na kueleweka kwa urahisi bila kumtatiza msomaji. Ikiwa basi ndiyo madhumuni, kuna haja gani kutumia lugha ya kigeni ili kuwaelezea wasomaji wako jambo wanaloweza kuelewa kwa lugha yao wenyewe ambayo wanaielewa vyema.

Mtu aelezeapo jambo kwa maandishi akitumia lugha yake mwenyewe anaelewa vyema na ambayo pia wasomaji wake wataielewa kwa ukamilifu. Kwa ujumla jambo ambalo mwandishi huyo ataliandika kwa

lugha ambayo ni ya asili yake ambayo anaelewa vyema, halitamtatiza msomaji wake ambaye pia anaelewa vyema lugha hiyo.

Maswali

a) Eleza mbinu zinazotumiwa na wakoloni kuwafanya wananchi kuidunisha lugha ya Kiswahili (alama 3)

.....

.....

.....

b) Thibitisha kuwepo kwa ukoloni mamboleo katika habari uliyosoma (alama 4)

.....

.....

.....

.....

c) Eleza jinsi wabeberu wanaweza kuzua vurugu katika mataifa mbalimbali (alama 2)

.....

.....

4. Taja sababu ambayo imewafanya wananchi wengi kupuuza lugha ya Kiswahili (alama 1)

.....

.....

5. Wakoloni wana mtazamo gani kuhusu lugha ya Kiswahili? (alama 2)

.....

.....

.....

6. Eleza maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumiwa katika taarifa (alama 3)

- i. Uadilifu.....
- ii. Akijitwaza.....
- iii. Waliotopea

2. UFUPISHO

Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali:

Mirundiko ya taka pamoja na utaratibu usiofaa wa uzoaji wake ni tisho kubwa kwa siha ya umma pamoja na mazingira. Hii ni kwa kuwa taka huwa na makaazi ya wadudu na wanyama waharibifu kama nzi, mbu, kombamwiko na panya ambao hueneza magonjwa na kuharibu vitu vyenye thamani. Maji taka nayo, pamoja na mifuko ya plastiki, huwa mastakimu ya wadudu na virusi vinavyoleta magonjwa mbalimbali. Mifuko ya plastiki ina madhara zaidi kwa kuwa huziba mitaro ya maji na kuzuia upitaji wa maji. Madhara hutokeza wakati mvua za gharika zinaponyesha. Maji hukosa njia yake ya kawaida ambayo huwa imezibwa na mifuko hii. Maji haya husababisha mafuriko ambayo huleta hasara ya mali na wakati mwingine ya uhai. Fauka ya haya, mifuko hii huwasakama tumboni wanyama sio wa nyumbani tu, bali wa porini na majini.

Kwa sababu ya hatari zitokanazo na taka, pana haja kutafuta njia na teknolojia ya kuweza kukabiliana na taka ili kuyatunza mazingira na siha ya umma. Njia mojawapo ya kufanya hivi ni kuelimisha na kuhimiza umma kuwa na uangalifu katika matumizi ya bidhaa na rasilimali ili kupunguza uzalishaji wa taka. Matumizi ya bidhaa kwa njia ya ubadhilifu huwa chanzo cha uzalishaji wa taka kwa wingi. Kwa mfano maji ni rasilimali ambayo imeendelea kutumiwa kwa ubadhirifu na hiyo huzalisha maji taka kwa wingi. Rasilimali hii inaweza ikatumiwa kwa uangalifu. Kwa mfano badala ya kutumia bafu ya mnyunyu kuogea, mtu anaweza kutumia maji ya karai.

Watu wengi huchukulia taka kuwa kitu kisicho na manufaa yoyote. Hawajui kuwa kwa kutumia teknolojia endelevu, taka nyingi zinaweza zikageuzwa na kuwa na manufaa mengi. Vijana wadogo sehemu za mashambani wanahitaji pongezi kwa kuwa na utambuzi huu. Wengi kwa kukosa hela za kununua mipira ya viwandani hutumia makaratasi na mifuko ya plastiki kutengeneza mipira wanayoitumia. Hii ni teknolojia endelevu ambapo taka hugeuzwa na kuwa na manufaa.

Baadhi ya wananchi wenye ubunifu nao wameanzisha miradi ya kuzoa takataka kutoka majumbani mwa watu. Hutoza ada fulani ya uzoaji, kisha huzipeleka taka hizi kule zitakakobadilishwa ili ziwe na manufaa. Mifuko na mabaki ya plastiki kama vile matangi, mitungi, sapatu na champali. Taka hizi huwa malighafi ya kutengenezea bidhaa nyingine. Taka za chupa na chuma nazo huuzwa katika viwanda vinavyozigeuza kuwa na manufaa tena. Taka za karatasi hutumiwa kutengenezea bidhaa kama vitabu, kтони, shashi za chooni, magazeti na kadhalika.

Taka zinaweza pia kugeuzwa kuwa zenye faida kwa kuzitumia kufanyia mboji. Ni muhimu kutambua kuwa si kila aina ya taka inaweza kutumiwa hapa. Taka zinazoweza kufanyiwa mboji ni zile ambazo huoza kwa haraka nazo ni kama vile mabaki ya vyakula, mboga na matunda. Kwa sadfa, hizi ndizo taka zinazozalishwa zaidi siku hizi na hasa sehemu za mjini na katika maeneo ya biashara kama mikahawa, hospitali n.k. Mtu akiwa na nafasi anaweza kuchimba shimo ambalo atafukia taka hizi ili kutengeneza mbolea. Hii ni njia isiyodhuru mazingira nayo ina manufaa kemkem. Kwanza, hugeuza taka ambayo

inaweza kuwa hatari na kuifanya iwe yenye manufaa. Kwa hivyo, hutatua matatizo ya kiafya yanayoweza kutokana na mirundiko ya taka. Mchanga nao hufaidika kupata virutubishi. Mbolea kama hii inaweza ikatumika kukuzia mboga au maua katika bustani.

Maji taka, hasa yanayotumiwa kuoshea vyombo, nayo yanaweza kutumika kunyunyizia mashamba madogo ya mboga au bustani za maua. Maji taka haya yanahitaji kutayarishiwa njia mahususi ya kuyaelekeza katika mashamba haya baada ya kutumiwa.

Aghalabu watu wengi wana mazoea ya kuchoma taka. Ni kawaida kupata matanuri ya kuchomea taka katika baadhi ya mitaa, shule, hospitali na kadhalika badala ya kupoteza moto bure inawezekana pakawekwa birika kubwa au tangi la chuma ambalo litatumia moto huo kuchemshia maji ambayo yanaweza kutumiwa katika shughuli za nyumbani.

Hata hivyo, ni muhimu kukumbuka kuwa kuna baadhi ya taka ambazo ni hatari na huenda zisigeuzwe ili kutumika kwa njia yenye faida. Taka hizi ni kama vile mikebe au vifaa vingine vyenye kubeba sumu au dawa hatari. Ni bora kuzitupa dawa hizi katika mashimo marefu au vyoo vya mashimo. Kwa vyovyote vile, si jambo muhali kuwa watu popote wanapoishi kulinda siha yao pamoja na kutunza mazingira. Ulinzi na utunzaji huu huhitaji uangalifu mkubwa katika utupaji taka.

MASWALI

- (a) Bila kupoteza maana iliyokusudiwa na mwandishi, **fupisha** aya ya kwanza na ya pili.

(Maneno 70)

(alama 7,1 ya mtiririko)

Matayarisho

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

Jibu

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

- (b) Kwa kuzingatia aya ya 3,4,5,6 na 7 **eleza** mambo muhimu anayoshughulikia mwandishi
(maneno 100– 120) (alama 8,1 ya mtiririko)

Matayarisho

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

Jibu

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

3. SEHEMU B: SARUFI NA MATUMIZI YA LUGHA (ALAMA 40)

- a. Andika neno moja lilo na mpangilio wa sauti zifuatazo: kikwamizo sikhuna cha ufizi, irabu ya mbele wastani, nazali ya midomo na irabu ya nyuma wastani. (alama 2)

.....

.....

- b. Eleza miundo ya silabi katika neno: **mbilikimo**. (alama 2)

.....

.....

.....

- c. Tunga sentensi ya **neno moja** iliyo na vipashio viifuatavyo vya kisarufi: kiima, kiambishi cha wakati ujao, shamirisho kitondo, mzizi, kauli tendea na kiishio. (alama 3)

.....

.....

.....

- d. Tunga sentensi moja kudhihirisha matumizi mawili ya kiambishi **i**. (alama 2)

.....

.....

.....

- e. “Akisa! Akisa! Mbona huitiki! Njoo hapa upesi!” mama alimwamrisha. (alama 3)

Andika kwa usemi wa taarifa:

-
-
-
- f. Waumini wa kweli humcha Maulana kila wakati. (alama 1)

Anza: Maulana...

.....

.....

- g. **Kanusha kwa udogo:** Ndovu huyu alimdhuru nguruwe huyo mchafu. (alama 2)
-
-

- h. Andika kunyume: Shamsi alilewa kisha akaukomea mlango wake usiku. (alama 1)
-
-

- i. Tunga sentensi moja yenye kiwakilishi cha A-unganifu, kitenzi kishirikishi kipungufu na kijalizo. (alama 3)
-
-

- j. Ziunganishe sentensi zifuatazo kwa kiunganishi cha masharti. (alama 2)
- Wakulima watapata mazao mazuri. Wakulima watazingatia kilimo cha kisasa.
-
-

- k. Tumia neno '**mpaka**' katika sentensi kama: (alama 3)

a. Nomino

b. Kihusishi

c. Kiunganishi

- l. Bainisha aina za vishazi tegemezi katika sentensi ifuatayo: (alama 2)

Kipakatalishi kilichonunuliwa jana kitatumiwa inavyotakiwa na mwenyewe.

.....

.....

.....

m. Ichanganue sentensi ifuatayo kwa visanduku: (alama 3)

Matandiko na Sisomi wataketi karibu na daraja.

.....

.....

.....

.....

.....

.....

n. Jibu kulingana na maagizo:

i. Kwetu kumenyesha mvua usiku kutwa na waongozi wakahairisha mikakati ya kuthibiti mmomonyoko wa udongo. (Sahihisha) (alama 2)

.....

.....

ii. Mwanariadha bora alipewa **zawadi** kisha akaandaliwa **karamu** katika ikulu. (Andika upya ukigeuza maneno yaliyopigiwa mstari kuwa vitenzi). (alama 2)

.....

.....

o. Bainisha shamirisho na chagizo katika sentensi ifuatayo:

Ajuza huyo alijengewa nyumba kwa matofali na mwanawe mara moja. (alama 2)

.....

.....

.....

.....

p. Tunasema simile tunapomba kupishwa, taib tunapo..... na

..... tunapotaka kitu kinusurike. (alama 2)

- q. Tunga sentensi moja yenye kirai elezi na kirai kihusishi. (alama 2)

.....

.....

.....

- r. Jamala ni kwa hisani, kaba ni kwa na ni
kwa mziwanda. (alama 2)

- s. Iainishe sentensi ifuatayo kwa kuzingatia dhamira. (alama 1)
- Meza tembe mbili mara tatu kila siku.

.....

.....

4. SEHEMU D: ISIMUJAMII (ALAMA 10)

- a. Fafanua dhana ya wingilugha. (alama 1)

.....

.....

- b. Eleza mambo manne yanayosababisha wingilugha. (alama 4)

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

- c. Fafanua sababu tano za watu kuhamisha na kuchanganya msimbo katika mawasiliano. (alama 5)

.....

.....

.....
.....
.....
.....
.....
.....
.....
.....
.....
.....

MOCK 1

102/2

KISWAHILI

KARATASI YA 2

LUGHA

MUDA : SAA 2 ½

JINA NAMBARI YA MTAHINIWA.....

SAHIHI YA MTAHINIWA TAREHE

MAAGIZO

- a) Andika jina yako na nambari yako katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.
- b) Tia sahihi yako kasha uandike tarehe ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa.
- c) Jibu maswali yote.
- d) Majibu yote yaandikwe katika nafasi ulizoachiwa katika kijitabu hiki cha maswali.
- e) Majibu yote lazima yaandikwe kwa Kiswahili.
- f) Usitoe ukurasa wowote kutoka kwenye kijitabu hiki.

KWA MATUMIZI YA MTAHINI PEKEE

SWALI	UPEO	ALAMA
1		
2		
3		
4		
JUMLA	80	

1.UFAHAMU (ALAMA 15)

Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswali:

Mwanamke wa kisasa anazaliwa na kukulia katika mazingira yaliyobadilika mno. Matazamio yake maishani ni tofauti na yale ya wanawake waliosihi mapote mawili yaliyopita; wanawake makamu ya nyanyake na mamake –kuu.

Yeye hatarajii kuzaliwa, kukua, kuolewa, kuwa mke wa bwana, kumzalia watoto, na daima dawamu kuwa **“mwandani wa jikoni”** akawapikia watoto na bwanake chakula; na akitoka jikoni aelekee shambani kulima, kichakani, kuchanja kuni,, mtoni kufua nguo na kuteka maji ya kutumia nyumbani. Mwanamke wa kisasa huandamana na mwanamume. **Akanyagapo mume naye papo huutia wayo wake.**

Mwanamke wa kisasa huenda shule na kujifunza yote yafunzwayo huko. Hushindana na wanawake kwa wanaume na kuibuka mshindi si mara haba. Huibuka mshindi katika masomo yake ya lugha, historia, jiografia, hesabu, sayansi na mengineyo, sawa na mwanamume.

Mwanamke wa kisasa hutaka kufanya kazi za kibega, akazifanya. Akitaka kuwa mwalimu, akawa. Akataka kuwa daktari, akafanikiwa. Almuradi, siku hizi mwanamke hufanya kazi yoyote ile afanyayo mwanamume. Kuna wanawake marubani wa ndege, masonara, waashi wahandishi, madereva wa magari, mawakili, mahakimu, mawaziri wakuu na hata marais wananchi. Hakuna kazi isiyoanywa na mwanamke siku hizi.

Mwanamke wa kisasa **hateswi akafyata ulimi**. Anapohiniwa yeye hupigania haki kwa dhati na hamasa. Katu hakubali’ mahali pake’ katika jamii alipotengwa na wanaume wenye mawazo ya kihaidhina yaliyopitwa na wakati.

Siku hizi mwanamke huolewa tu wakati amepata kazi ya kumwezesha kujikimu maishani au pale anapokuwa na hakika kwamba biashara yake, iwapo ni mfanyi biashara, imepiga hatua ya kutomrudisha **ukutani**.

Mwanamke wa kisasa haamuliwi katika jambo lolote, bali hufanya maamuzi yake mwenyewe. Kwa upande mwingine, mwanaume wa ‘kisasa’, ambaye bado amefungwa pingu na taasubi za kiume, hapendezwi na mwanamke huyu. Huuma kidole akatamani yale ya akale, lakini wapi! Analazimika kukubali mwanamke huyu kama mshirika sawa maishani, na kuishi naye, apende asipende. Shingo upande analazimika kukubali kwamba mabadiliko haya sio mithili ya kiwingu kipitacho, bali ni ya **aushi**.

MASWALI

a)Msemo '**mwendani wa vijungu jiko**' unadhihirisha hali gani ya mwanamke katika jamii? (al.2)

.....

.....

.....

b)Jamii imefanya mwanamke kuwa hayawani wa mizigo. Fafanua. (al.2)

.....

.....

.....

c)Eleza maana ya '**akanyagapo mume papo huutia wayo wake**' (al.2)

.....

.....

d)Mlinganishe mwanamke wa kiasili na wa kisasa katika maswala ya ndoa na elimu. (al.4)

.....

.....

.....

.....

.....

e)Mwanamume wa kisasa anamwonaje mwanamke wa kisasa? (al.2)

.....

.....

.....

f)Eleza maana ya:

(i)Akafyata ulimi (al.1)

.....

(ii)Ukatani (al.1)

.....

(iii)Taasubi za kiume (al.1)

.....

2.MUHTASARI / UFUPISHO

Soma kifungu kisha ujibu maswali.

Imesemekana na kurudiwa tena na tena kwamba, iwapo tuna maono ya kujiondoa katika umaskini wa kupindukia, ni lazima tukipe kilimo umuhimu. Zaidi ya Wakenya milioni kumi wamo katika hatari ya kufa katika maeneo mbali mbali kwa sasa kufuatia uhaba wa chakula nchini.

Kiini kikubwa cha njaa hiyo ni mapuuza ya muda mrefu katika sekta ya kilimo.Imesahaulika kuwa karibu asilimia sabini na tano ya Wakenya wanategemea kilimo kwa chakula na mapato ya kifedha kila siku. Kilimo hutoa karibu robo tatu ya nafasi za kazi kwa wananchi na pia kuletea serikali karibu robo ya mapato yake kutokana na mauzo ya mazao katika mataifa ya nje.

Wataalamu wa maswala ya zaraa wanaeleza kuwa pato la nchi linatokana na kilimo huangamiza njaa mara nne zaidi ya mapato yanayotokana na shughuli nyinginezo za kiuchumi. Hiyo ni kwa sababu shughuli za kilimo hulenga kuzalisha vyakula moja kwa moja.

Imebainika kuwa, katika mataifa mengi yanayostawi, asilimia sabini na tano ya wananchi huishi katika maeneo ya mashambani na idadi hii hutegemea kilimo kujimudu kimaisha ilhali hapa Kenya ni asilimia nne pekee ya bajeti inayowekezwa katika kilimo.Kwa wakati huo, ushuru unaotowza bidhaa za kilimo katika maeneo haya umebainika kuwa mkubwa. Hii imepelekea uwekezaji katika kilimo kupungua na hivyo kuchangia kukithiri kwa baa la njaa.

Wakati umewadia kwa serikali za Afrika na wapangaji wa masuala ya uchumi kuweka juhudi maradufu katika kushabikia ili kumaliza njaa na umaskini. Kuna haja ya kuwajulisha, kuwahimiza na kuwaelimisha wakulima wa mashamba madogo madogo kuhusu mihimili ya zaharaa kama vile uzalishaji wa matunda na mboga, ufugaji wa ndege, samaki na ng'ombe mbali na kuweka mikakati ya kuanzisha nafasi za kazi katika sekta ya kilimo.

Serikali itafikia lengo hili iwapo itaanza kufadhili kilimo, kupunguza gharama za pembejeo za kilimo, kuweka sera zinazodhibiti uuzaji na ununuzi wa vyakula hasa baina ya mataifa na kuongeza sehemu ya bajeti inayotengewa kilimo. Bila hilo hatutakuwa na lingine bali kukimbilia mataifa yalistawi kuomba misaada ili kuwanusuru raia wetu kutokana na ghadhabu na njaa.

a)Fupisha aya mbili za mwanzo (maneno 50 – 55) (al.6, 1 ½ ya mtiririko)

Matayarisho

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

Nakala safi

.....

.....

.....

.....

.....

.....

(b)Bila kubadili maana,fupisha aya mbili za mwisho. (maneno 55 – 60) (al.6, 1 ½ utiririko)

Matayarisho

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

Nakala safi

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

3.MATUMIZI YA LUGHA (ALAMA 40)

a)Taja sauti zenye sifa zifuatazo. (al.2)

i)Irabu ya mbele, juu, tandazwa.

.....

ii)Kiyeyusho cha midomo.

.....

b)Tofautisha kati ya silabi funge na silabi wazi na utolee mifano. (al.2)

.....

.....

.....

.....

c)Eleza dhima ya sentensi ifuatayo. (al.1)

Naomba uniazime kalamu yako.

.....

.....

d)(i)Eleza maana ya mofimu. (al.1)

.....

.....

.....

(ii)Ainisha mofimu katika neon

alani? (al.2)

.....

e)Tambua aina za vitenzi katika sentensi ifuatayo: (al.3)

Hawa sio walimu bali wamekuwa wakifunza katika shule hii.

.....

.....

.....

.....

f)Weka neno hili katika ngeli mbili tofauti : (al.2)

Maziwa

.....

g)Eleza tofauti iliyopo kati ya ukanushaji na kinyume. (al.2)Andika kinyume cha

Kibe alikunja nguo zilizoangikwa ukutani alama 1

.....

Kanusha

Kibe alikunja nguo zilizoangikwa ukutani alama 1

.....

h)Andika katika wingi: (al.2)

Zigo la kuliwa halilemei.

.....

.....

i)Andika sentensi ifuatayo katika hali ya udogo wingi. (al.2)

Meza ilianguka ikavunjika tendeguu.

.....

)Tunga sentensi mojamoya ukitumia vitenzi vifuatavyo katika kauli ulizopewa mabanoni. (al.2)

Paka (tendata)

.....

Choma (tendua)

.....

k)Tumia nomino mji kama kielezi cha mfanano. (al.1)

.....

.....

l)Tunga sentensi mbili kuonyesha maana tofauti za neno walakini na uzitaje. (al.2)

.....

.....

.....

.....

m)(i)Tunga moja sentensi ambatano.(al.2)

.....

.....

(ii)Changanua sentensi ifuatayo kwa njia ya matawi . (al.4)

Mbwa pamoja na paka walikuwa wakiuzwa sokoni.

n)Ainisha virai katika sentensi ifuatayo:

Wote wanne walijificha nyumba ya mlango.

.....

.....

.....

o)Onyesha aina za vishazi katika sentensi ifuatayo. (al.2)

Babake alipofika nyumbani alipumzika kitandani.

.....

.....

.....

p)Andika sentensi moja yenye shamirisho zifuatazo. (al.3)

kipozi, kitondo na ala.

.....

.....

q)Andika sentensi ifuatayo katika msemu wa taarifa.

“Tutawapa zawadi zenu kesho mkija na wazazi,” mwalimu aliwaambia.

.....

.....

.....

r)Andika upya sentensi ifuatayo ukitumia kisawe cha neno lililopigiwa mstari. (al.1)

Babangu hapendi kunywa pombe.

.....

.....

s)Tofautisha sentensi. (al.2)

(i)Ungalisoma kwa bidii, ungalipita mtihani.

.....

.....

ii)Ungelisoma kwa bidii, ungelipita mtihani.

.....

.....

4. ISIMU JAMII (ALAMA 10)

“Naona ‘Horse Power’ mwenyewe ndiye atakayepiga,..... atakayecheza foul hiyo. Wachezaji wa

a)Tambua sajili inayorejelewa. (al.2)

.....

.....

.....

b)Tambua sifa zinazobainisha sajili yenyewe. (al.8)

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

POST MOCK 1

JINA _____ TAREHE _____

SHULE _____ NAMBA YAKO _____

SAHIHI _____

102/2

KISWAHILI: LUGHA

MUDA: SAA 2½

Hati ya Kuhitimu Mtihani wa Kitaifa wa KCSE

102/2

KISWAHILI: LUGHA

MUDA: SAA 2½

MAAGIZO KWA MTAHINIWA

- Karatasi hii ina kurasa kumi na moja zilizopigwa chapa.*
- Andika jina na nambari yako katika nafasi ulioachiwa hapo juu.*
- Jibu maswali yote.*
- Majibu yote yaandikwe katika nafasi zilizoachwa katika kijitabu hiki cha maswali.*
- Majibu yote yaandikwe katika lugha ya Kiswahili.*

KWA MATUMIZI YA MTAHINI PEKEE

SWALI	UPEO	ALAMA
1	15	
2	15	
3	40	
4	10	
JUMLA	80	

Watahiniwa ni lazima wahakikishe kwamba kurasa zote za karatasi hii zimepigwa chapa sawasawa na kuwa maswali yote yamo.

1. UFAHAMU (ALAMA 15)

Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali yanayofuata.

Ilikuwa jumamosi. Nilifika nyumbani kwangu saa moja jioni. Tangu nistaafu miaka miwili awali sikupenda kuchelewa kusikiliza taarifa ya habari.

Mwezi mmoja ukawa umepita tangu nipewe kiinuamgongo. Mwezi mmoja mzima nilikuwa katika shughuli za kulipa deni hapa na kulipa karo huku. Kuwekeza kwenye mradi ule na kununua hili. Sasa shilingi laki mbili tu zilikuwa zimesalia katika benki.

Watu wengi walinishawishi nijaribu kilimo cha mahindi. Bei ilikuwa imeanza kuimarika. Katika taarifa ya habari jioni hiyo, waziri wa kilimo alitangaza bei mpya. Shilingi 1,500 kwa kila gunia la kilo tisini. Nami nilikuwa naanza kuumakinikia mradi huu.

Baada ya taarifa, nilikoga, nikala na nikaenda kulala. Kwa sababu ya uchovu, usingizi ulinichukua mara moja. Usingizini niliota. Katika ndoto niliutekeleza mradi wangu. Msimu huo wa kulima nilitenga ekari kumi za shamba langu. Wataalamu walinishauri kuwa wakati mzuri wa kulima ni wakati wa kiangazi. Mwezi wa Januari ulipoanza tu nilitafuta trekta na kulima. Malipo yalikuwa shilingi 1,200 kila ekari. Katikati ya mwezi wa Machi, nilitafuta trekta la kutifua shamba tena kwa gharama ya shilingi 15,000 ekari zote kumi. Kufuatia ushauri wa manyakanga wa kilimo, nililipa shilingi elfu kumi na tatu kupiga shamba lote haro.

Mwishoni mwa mwezi huo, nilienda mjini kutafuta pembejo. Kwanza, nililipa shilingi 20,500 kwa magunia 15 ya mbolea. Kisha nilinunua magunia manne ya mbegu ya mahindi yenye uzani wa kilo 25 kwa shilingi 3,300 kila gunia. Mwezi wa Aprili ulipotimia tu, niliamua kupanda. Ili nipate mazo bora, nilipanda kwa tandazi. Gharama ilikuwa shilingi 1,000 kila ekari. Mvua ilinyesha vizuri na baada ya siku saba, mahindi yalianza kuota. Ilifurahisha kuhesabu mistari ya kijani iliyonyooka. Hali hii iliwezekana tu baada ya kuajiri vijana wa kuwafukuza korongo na vidiri ili wasifukue mbegu mchangani.

Baada ya mwezi mmoja, hatua ya kupalilia ilifika. Nilitafuta vibarua na kupalilia. Malipo yalikuwa shilingi 700 kila ekari. Kumbe kupalilia kulichochea mtifuko wa mahindi. Punde yakawa yananifikia magotini. Hii ikawa ishara

kuwa yanahitaji kumwagiwa mbolea ya kunawirisha iitwayo ‘amonia’. Gharama yake ikawa shilingi 1,300 kila gunia. Hivyo nikalipa shilingi 19,500 kwa magunia kumi na matano.

Mahindi yalibadilika kimiujiza. Ghafla tu yalirefuka na kunenepa mashina. Yalibadilika rangi yakapiga weusi. Shamba liligeuka likawa kama msitu wa rangi ya kijani iliyokolea. Wapitanjia walijababua mimea na juhudi zangu. Shamba langu sasa likawa kielelezo. Maafisa wa kilimo wakawa kila siku wanaleta wakulima wengine kujifunza siri ya ufanisi wangu. Hapo nikaanza kuhesabu mavuno nitakayopata na kukadiria faida. Nilipuuza kabisa ushauri wa wahenga kuwa ‘Usikate majani, mnyama hajauawa.’

Bila taarifa wala tahadhari, mvua ilitoweka. Hayakupita majuma mawili mahindi yakaanza kubadilika. Juma moja baadaye mahindi yalinyauka. Badala ya mahindi, shamba likageuka la vitunguu vilivyochomwa na jua. Makisio yangu ya faida yaliyeyuka jinsi ufanyavyo moshi. Lakini ‘Muumba ndiye Muumbua.’ Siku moja mawingu yalitanda na mvua ikanyesha. Muda si muda mahindi yalianza kunawiri. Kumbe tuko lililonivunja moyo lilikuwa laja. Siku moja mvua kubwa ilinyesha. Asubuhi nilipotoka nje nilipigwa na butwaa. Barafu ilitapakaa pote. Shamba lilikuwa limetapakaa barafu huku majani ya mahindi yamechanika kama nyuzi. Niliugua. Baada ya wiki moja, nilipata nafuu. Nilipotazama upande wa shamba niliona dalili za majani mapya ya mahindi yakianza kuchomoza. Maumbile ni kitu cha ajabu kweli.

Muda si mrefu mahindi yalirudia hali yake tena, kisha yakakomaa. Harakati za kutafuta watu wa kuyakata na kuyakusanya zilianza. Gharama ya shughuli hii ikawa shilingi 5,000. Kuvuns, kusafirisha kutoka shamba na kukoboa kwa mashine magunia 200 yakachukua shilingi 20,500. Kufikia hapo nilikuwa nimetumia takribani shilingi 192,700. Gharama nyingine zilikuwa za usafiri, gharama ya dharura na usimamizi, usumbufu wangu binafsi, gharama ya magunia na kadhalika. Mahindi yalipokuwa tayari kwenye magunia nilifunga safari kwenda mjini kutafuta soko. Niliposhuka tu niliona gazeti. Habari motomoto siku hiyo ilikuwa. ‘MAHINDI GUNIA 900/=.’ Niligutuka usingizini.

Maswali

(a) Andika kichwa mwafaka kwa kifungu hiki cha habari. (alama 1)

(b) Msimulizi alikuwa na kiasi gani cha pesa katika benki baada ya mradi kukamilika? (alama 2)

(c) Taja matatizo matatu yaliyotishia mradi wa msimulizi wa kukuza mahindi (alama 3)

(d) Eleza maana za methali zifuatazo kwa mujibu wa taarifa

(i) Usikate majani, mnyama hajauawa (alama 1)

(ii) Muumba ndiye muumbua (alama 1)

(e) Eleza mambo mawili yaliyosababisha msimulizi asipate faida alivyotarajia. (alama 4)

(f) Kwa nini msimulizi alisema maumbile ni kitu cha ajabu? (alama 1)

(g) Eleza maana za;

i. Kinuamgongo (alama 1)

2. UFUPISHO(ALAMA 15)

Soma makala yafuatayo kisha ufupishe kwa mujibu wa maswali uliyopewa. Utafiti umebaini kuwa pana uwiano baina ya lugha inayotumiwa kwa lugha rasmi na kiwango cha umaskini katika nchi, na pia kiwango cha ustawi. Kwa mfano, nchi nyingi za Afrika zimekuwa zikitumia lugha za wakoloni waliozitawala kama lugha rasmi. Nchi hizi zimekuwa zikitumia lugha hizo katika shughuli rasmi, kutoa mafunzo na kupitishia sera muhimu zinazoathiri maisha ya wananchi wote. Kile wasichozingatia ni kuwa, raia wao wengi hawazielewi.

Idadi kubwa ya raia barani Afrika ni wakulima au wasakatonge katika sekta za juakali, uchukuzi na biashara ndogondogo ambao hawana umilisi wa lugha hizo za kigeni. Watu hawa aghalabu huendesha shughuli zao za kila siku kwa kutumia lugha zao za asili, au kama hapa Afrika Mashariki, hutumia Kiswahili ambacho aghalabu hawazingatii usanifu wake. Je, kwa nini tusiokoe na kuauni idadi hii kubwa ya watu ili kuimarisha hali zao kiuchumi, kijamii na ambazo hawazielewi; lugha zinazotumiwa na kufahamika na wachache?

Manufaa ya kutumia lugha inayoeleweka ma kufahamika na wengi kama lugha rasmi ni lukuki yakilinganishwa na maumizi ya lugha za kigeni kama kiingereza, kifaransa, kijerumani au kimandarin. Kwanza, matumizi yake huwawezesha watumiaji kujieleza wakaeleweka vizuri kwa kuwa mkondo wa fikra unatumia lugha wanayoiua, na hivyo wana nafasi ya kuwa wabunifu. Kwa mfano, matumizi ya lugha asili katika utoaji elimu yatahakikisha kuwa wanafunzi wanashiriki kikamilifu katika shughuli zote za kielimu. Hawatakuwa wanafunzi wanaongojea kuelezwa kila kitu bali watajisakuria ili kujizidishia maarifa.

Matumizi ya Kiswahili, lugha inayoeleweka na idadi kubwa ya watu, huhakikisha kuwa ujuzi na maarifa yanayopitishwa si himaya ya kundi dogo tu lililoelimika bali hata wale wasiobahatika kuzielewa lugha hizo za kigeni. Hii ni

kwa sababu anayesema kwa lugha ya kigeni husema na ubongo, naye asemaye kwa lugha asili husema na moyo, hivyo basi akaeleweka zaidi katika yale ayasemayo. Aidha, matumizi haya hutoa nafasi sawa kwa wengi na kuepusha utegemezi wa wakalimani ambao aghalabu hawaeleweki kutokana na kasi ya mazungumzo, au wakatoa fasiri isiyo sahihi. kila mmoja ataweza kushiriki kikamilifu katika ujenzi wa taifa kutokana na uwezo wa kufasiri sera za serikali na kutoa uamuzi wao wenyewe ikilinganishwa na wakati ambapo sera hizi zinawasilishwa kupitia lugha za kigeni.

Fauka ya haya, matumizi ya lugha inayoeleweka na wengi huwawezesha watu kushiriki na kuchangia katika uimarishaji wa demokrasia kutoka vijijini, hadi kitaifa. Hata hivyo, itashangaza kumwona mzungu akizungumza na wanajamii kwa Kiswahili, naye mwakilishi wa jamii hiyo akiwazungumzia kwa kiingereza. Hii ni njia mmoja ya kuwatenga raia wasioelewa lugha hiyo ya kigeni. Matumizi ya lugha kama hii huhujumu mtagusano baina ya watu. Kwa hivyo, hakisalii tu kuwa lugha rasmi katika katiba bali katika uhalisia.

Maswali

(a) Fupisha aya ya kwanza kwa kutumia maneno 35-40

(alama 5)

Nakala chafu

Nakala safi

(b) Kwa maneno kati ya 100-110, eleza manufaa ya kutumia lugha inayoeleweka
na watu wengi kama lugha rasmi katika nchi. (alama 10)

Nakala chafu

Nakala safi

3. SARUFI NA MATUMIZI YA LUGHA (ALAMA 40)

(a) Taja vipasuo viwili vya kaakaa laini. (alama 2)

(b) Andika neno lenye sauti mwambatano. (alama 1)

(c) Weka shadda katika neno lifuatalo ili itoe maana mbili tofauti. (alama 2)
ala

(d) Tumia kiimbo katika sentensi mbili tofauti ili kudhihirisha. (alama 2)
i. Ombi/rai

ii. Amri/kuamuru

(e) Tambulisha vipashio vinne vya sarufi ya Kiswahili. (alama 2)

(f) Tunga sentensi kwa kutumia kiwakilishi huru nafsi ya tatu wingi. (alama 2)

(g) Tumia kivumishi cha pekee katika sentensi kuonyesha umilikaji. (alama 1)

(h) Tumia vihusishi kuonyesha uhusiano wa wakati na kiwango. (alama 2)

(i) Weka maneno haya katika ngeli zake. (alama 2)

i. Miwani

ii. Wema

(j) Ainisha mofimu katika neno lifuatalo. (alama 3)
Hakuwakaribisha

(k) Bainisha tofauti kati ya mzizi huru na mzizi funge kwa kutoa mifano. (alama 2)

(l) Bainisha kishazi huru na kishazi tegemezi katika senensi ifuatayo. (alama 2)
Utakapomkabidhi barua hii, nipashe habari

(m) Tambua aina za shamirisho katika sentensi ifuatayo. (alama 3)
Ilitumwa kumlimia nyanya shamba

(n) Yakinisha sentensi ifuatayo katika hali ya mazoea. (alama 2)
Hakuwasaidia wala hakuwakaribisha kwake.

(o) Tambua kirai kihusishi katika sentensi ifuatayo. (alama 1)
Jino la Tamma linauma mara kwa mara.

(p) Tunga sentensi ukitumia neno zawadi kama kitenzi (alama 2)

(q) Andika katika usemi wa taarifa. (alama 2)
“Nitamwalika mtondogoo.” Fatuma akasema.

(r) Changanua sentensi hii kwa kutumia matawi. (alama 4)
Darasa lilojengwa limefunguliwa leo alasiri.

(s) Kanusha (alama 1)
Sisi ndisi wanafunzi

(t) Tunga sentensi moja ukitumia kiambishi –po- kudhihirisha mahali dhahiri. (alama 1)

4. ISIMU JAMII (ALAMA 10)

(a) Eleza maana ya lugha ya taifa. (alama 2)

(b) Eleza sababu tatu zinazofanya watu kubadili na kuchanganya ndimi. (alama 3)

(c) Eleza hatua tano ambazo zimesaidia kukuza lugha ya Kiswahili baada ya uhuru nchini Kenya. (alama 5)
